

SEMINA YA WAZEE, NA MASHEMASI WA KANISA KUONGOZA IBADA

Utangulizi Ni nini maana ya neno ibada?

Matumizi ya kawaida na ya jumla; Ibada ni mkusanyiko wa watu kwa kufanya shughuli za ibada, kwa wakristo in maana mikusanyiko ya maara kwa mara kanisani mikusanyiko ya juma kwajuma, siku kwa siku. Neon la kigiriki “**Proskuneo**”(kuabudu) kuabudu ina maana kuonyesha tendo la heshima ya hali ya juu linalotolewa kwa Mungu pamoja na kusifu kwa uweza wake mkuu.

Heshima kwa Nyumba ya Mungu

“Tulieni mbele za BWANA, enyi watu wote, kwa sababu ameinuka kutoka makao yake matakatifu.” **Zekaria 2:13**

Kama ungetembelea mmoja wa wafalme wa dunia hii katika jumba lake la kifalme,

- Fikiria kwenda ovyo ovyo mbele zake
- Fikiria kama hukuvaa vizuri na mavazi yako ni machafu
- Fikiri juu ya kufungua na kufunga milango kwa fujo
- Fikiri juu ya kucheka cheka na kusema bila adabu mbele za mfalme

Bila shaka hungeruhusiwa kuendelea kuongea na mfame na ungeondolewa mara moja, hiyo ni heshima ya dunia hii tu ambayo wanastahili wafalme ambao ni wanadamu wenzetu.

“Na hao wenye uhai wane wanapompa yeye aketi juu kiti cha enzi utukufu, na heshima na shukrani yeye aliye hai hata milele na milele ndipo hao wazee ishirini na wane huanguka mbele zake yeye Yule aketiye juu ya kiti cha enzi, nao humsujudia yeye aliye hai hata milele na milele nao huzitupa taji zao wakisema umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu kuupokea utukufu na heshima na uweza kwa kuwa wewe ndiye uliyeviumba vitu vyote na kwa sababu ya mapenzi yako vikaumbwa vilikuwako navyo vikaumbwa. utukufu na heshima na uweza.”

Yohana alionyeshwa tendo la ibada mbinguni

- a) Alionyeshwa kiti cha enzi ameketi mtu mfano almasi na jiwe zuri jekundu, amezungukwa na upinde wa mvua unaong’aa sana kama zumaridi
- b) Wenye uhai wanne mchana na usiku humpa Mungu utukufu na heshima mchana na usiku
- c) Wazee ishirini na nne waliovaa mavazi meupe na taji vichwani mwao wakimsujudu Mungu na kutupa taji zao mbele zake wakitoa sifa na heshima Ufunuo 4:1-11

Zaburi 89:7 Mambo Matatu Makuu Ili Ibada yetu Iweze Kumpendeza Mungu

1) Kicho, Utii na unyenyekevu kwa waabudu wote

Ikiwa watu wanakuja katika katika nyumba ya ibada, watakuwa na kicho cha kweli kwa Bwana na kukumbuka kuwa wako mbele zake, kutakuwa na ushawishi katika kimya. Kunong'ona na kucheka, nakuzungumza ambavyo vinaweza visiwe kosa katika sehemu za shughuli za kawaida visiruhusiwe kabisa katika nyumba ambamo Mungu anaabudiwa. Akili ni lazima iandaliwe kusikiliza neon la Mungu ili liweze kuwa na uzito unaostahili na kugusa moyo. **5Testimonies 491,492**

2) Kujitawala, kujitakasa na kwa waongoza ibada

“Wachungaji na wazee wa kanisa ambao wangeweza kufanya kazi na kufanikiwa kwa ajili ya wokovu war oho za watu hawana budi kuwa wanafunzi wa Biblia na watu wenye kumwomba Mungu. **Ni dhambi kuacha kusoma neno la Mungu na huku tukijaribu kulifundisha kwa wengine.** Wale wanaoona thamani ya roho za watu hufahamu kuwa ni hatari sana kwao kuthubutu kutojali maendeleo yao katika ujuzi wa mambo ya Mungu.” **Wajumbe wa Kristo uk 28**

“... Ujumbe wangu kwa wachungaji vijana na wazee ni huu, angalieni kwa uangalifu sana saa zenu za maombi kusoma Biblia na kujihoji nafsi. Wekeni nafsi kila siku kwa ajili ya kusoma maandiko matakatifu na kushirikiana na Mungu. Hivyo ndivyo mtakavyopata nguvu za kiroho nanyi mtakuwa na kupata kinbali kwa Mungu.” **Ibd uk 29**

3) Wachungaji na Wazee wa Kanisa Kusimamia utaratibu wa Ibada

Hapa ku vipengele ambavyo wachungaji na wazee wa kanisa wapaswa kuvisimamia

- Katika kupanga hakikisha wahudumu wa ibada wawe wale walioruhusiwa
 - Watu walioondolewa ushirika wasiruhusiwe ibada
 - Wachungaji walioondolewa kazini wasiruhusiwe kuendesha ibada mpaka kwa ruhusa ya Conference au kama ni mshiriki mahalia
 - Wageni wasiruhusiwe kuendesha ibada
 - Wanakwaya wachaguliwe wale wanaofaa kuendesha ibada ya muziki muziki unafaa uendane na mada iliyoandaliwa.

Kabla ya huduma yoyote ya ibada watu, wanaohusika kusimamia nilazima wajulishwe jukumu lao mapema na kupewa muda wa kutosha ili wajiandae. Ikiwezekana kuwe na ratiba inyojulikana kwa wahudumu wote Lakini mambo yote yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu.

Mchungaji asipokuwapo ni wajibu wa mzee wa kanisa kuhakikisha kwamba kanuni hii inafuatwa. Mwongozo wa Mzee wa Kanisa uk181, 182

“Viongozi wa ibada wanapaswa kujikumbusha daima juu ya “utakatifu wa ibada ya Kikristo” na kuingia katika huduma yao kwa kicho cha Bwana na unyenyekevu, wakiomba kwamba Mungu awatumie wakati wakiongoza ibada. Watakataa kushindwa na misongo ya kiutamaduni ya kuhafifisha ibada. Wataweka kielelezo cha kicho cha hali juu na furaha ya ajabu wakati wakiongoza ibada. Mahubiri yasiharibiwe na kufanywa kama maelezo ya kawaida. Mazungumzo yasianguke katika mtego wa yasiyopasa na uimbaji kamwe usiwe maonyesho kwa watu. Ibada ya kweli sharti daima iwe sadaka kwa Mungu isiyo na ubinafsi. Kwa upande mwingine, viongozi wazuri wa ibada watakataa pia kuwa ving’ang’anizi kwa mapokeo bila sababu yoyote ya msingi. Badala yake, kicho chao kwa Mungu kitajidhihirisha katika heshima na hisia ya unyenyekevu wa juu.” 5Testimonies 495, 496.

Tahadhari yapo mambo kadhaa tunayoendesha kimakosa katika ibada- tunaharibu ibada

- I. Matangazo marefu
Matangazo yanapokuwa marefu yanachosha, mpango ungefanywa ili matangazo yachapishwe katika kijarida au kama ni machache na ikiwa inafaa yaunganishwe yawe ni sehemu ya ibada
- II. Mahubiri marefu
- Mahubiri marefu yaliyojaa falsafa na visa vya kuchekesha yanachocha, na hayajengi sana kwa waabudu wa kweli. Daima mahubiri yetu kiini chake iwe ni Kristo
- III. Maombi marefu
- Sala huelekea kuwa ndefu, sio kwa sababu tunayo mengi sana ya kusema bali ni kwa sababu hatuna mpangilio na tunalisema jambo kwa kurudiarudia. Roho ya unabii inasema Dakika moja au mbili ni nyingi kiasi cha kutosha kwa ombi la kawaida. 2Testimonies uk 581
- IV. Kwaya dhaifu
- Muziki unaowasilishwa kwa namna nzuri, huwa na mvuto wa nguvu sana katika kuinua mioyo kwa Mungu. Ni sehemu ya ibada kama ilivyo maombi. Kwa kweli uzoefu ulioandikwa katika nyimbo za Kristo na waandishi wa nyimbo hugeuka kuwa maombi ya waabuduo wanapokuwa wakiimba

Hitimisho

Kuongoza ibada ni mwito mkuu, na ni kwa neema ya Mungu tu ndipo unaweza kutekeleza kwa ufanisi mkubwa. Mungu, kupitia kwa Neno lake, anatupatia kanuni na miongozo bayana. Kama viongozi wa ibada, imetupasa kuifanya ibada kipaumbele chetu. Kama viongozi wa ibada, tusiishie katika kujenga sanaa ya ibada, tujenge pia mioyo kwa ajili ya ibada. Ni baada ya hapo tu ndipo tutaweza kuwasaidia waumini kuwa waabudu bora. Ni baada ya hapo tu ndipo tutuweza kumtolea Mungu ibada anayostahili. Hebu Mungu atujalie macho ya kuona ukuu wa

Na J. Lusega – Idara ya Uchapishaji (NETC)